**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**TAARIFA KWA UMMA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ZOEZI LA UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO, VYUO VYA UALIMU, VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI NA KATI KWA MWAKA 2023

**Ndugu Wanahabari;**

Zoezi la Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari, Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Kati vya Serikali Mwaka 2023, limekamilika. Zoezi hili limefanyika kwa kuzingatia takwimu za matokeo ya Wanafunzi waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne Mwaka, 2022, kutoka Tanzania Bara. Wanafunzi waliochaguliwa ni kutoka Shule za Serikali, zisizo za Serikali, watahiniwa wa kujitegemea waliofanya mtihani chini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

**Ndugu Wanahabari;**

Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka, 2022 yanaonesha kuwa Watahiniwa **192,348** (36.95%) walipata ufaulu wa Daraja la I – III**.** Kati ya hao Tanzania Bara walikuwa watahiniwa **188,128** wakiwemo wasichana **84,509** na wavulana **103,619**. Wanafunzi hawa wote wamekidhi vigezo vya kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya ualimu,Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Kati kwa mwaka, 2023. Idadi hii inajumuisha Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum **490** ambao wasichana ni **218** na wavulana ni **272**.

Wanafunzi wote **188,128** waliokidhi vigezo wamechaguliwa na kupangiwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule mbalimbali nchini pamoja na Vyuo vya fani mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Wanafunzi **129,830** wakiwemo wasichana **66,343** na wavulana **63,487** sawa na asilimia **69** ya wenye sifa, wamechaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za Kidato cha Tano kwa mchanganuo ufuatao,

(i) Wanafunzi **1,878** wakiwemo wasichana **1,097** na wavulana **781** wamepangiwa katika Shule za sekondari Maalum **8** za

Kilakala, Mzumbe, Ilboru, Kisimiri, Msalato, Kibaha, Tabora Boys na Tabora Girls.

(ii) Wanafunzi **122,908** wakiwemo wasichana **62,731** na wavulana **60,177** wamepangiwa katika shule **519** za Sekondari za Bweni za Kitaifa za Kidato cha Tano.

(iii) Wanafunzi **5,044** wakiwemo wasichana **2,515** na wavulana **2,529** wamepangwa katika Shule **11** za Sekondari za Kutwa za Kidato cha Tano.

(b) Wanafunzi **58,298** wakiwemo wasichana **18,166** na wavulana **40,132** sawa na asilimia **31** wamepangiwa kujiunga kwenye kozi mbalimbali za Stashahada katika Vyuo vya Kati vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET) katika mchanganuo ufuatao:

(i) Wanafunzi **1,645** wakiwemo wasichana **646** na wavulana **999** wamechaguliwa kujiunga na Vyuo vya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Sayansi, Hesabu na TEHAMA.

(ii) Wanafunzi **1,877** wakiwemo wasichana **757** na wavulana **1,120** wamechaguliwa kujiunga na fani mbalimbali katika Vyuo **04** vya Elimu ya Ufundi ambavyo ni Chuo cha Ufundi cha Arusha (**ATC**), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (**DIT**), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST na Chuo cha Usimamizi na Maendeleo ya Maji (WDMI).

(iii) Wanafunzi **1,842** wakiwemo wasichana **943** na wavulana **899** wamechaguliwa kujiunga na Vyuo vya Afya ngazi ya Stashahada.

(iv) Wanafunzi **52,934** wakiwemo wasichana **15,820** na wavulana **37,114** wamechaguliwa kujiunga kwenye kozi mbalimbali zikiwemo za Kilimo, Ufugaji, Utawala, Biashara na zinginezo za Stashahada katika Vyuo vya kati mbalimbali nchini.

**Ndugu Wanahabari;**

Muhula wa kwanza kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano utaanza tarehe **14 Agosti, 2023. Hivyo, Wanafunzi wote waliopangwa kujiunga na Kidato cha Tano kwa mwaka, 2023 wanapaswa kuanza kuripoti Shuleni kuanzia tarehe 13 Agosti, 2023**. Siku ya mwisho ya kuripoti itakuwa tarehe **31 Agosti, 2023.**

Fomu za maelezo ya mahitaji ya kujiunga na Kidato cha Tano *(Joining Instructions)* kwa Shule zote za Kidato cha Tano zinapatikana kwenye tovuti ya OR-TAMISEMI kupitia kiunganishi cha www.tamisemi.go.tz .

**Ndugu Wanahabari;**

Kwa wanafunzi waliopangwa kwenye Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi watapokea maelekezo ya namna ya kujiunga kutoka Vyuo walivyopangwa.

**Ndugu Wanahabari;**

Uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu ya Ufundi umefanyika kwa kuzingatia ufaulu na nafasi zilizopo katika Shule; hivyo, **hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya Shule kutokana na ukosefu wa nafasi.**

**Ndugu Wanahabari;**

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza walimu, wazazi na walezi wote kwa juhudi walizozifanya katika ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufaulu vizuri. Naomba wazazi/walezi wote tuendelee na moyo huu wa kusimamia na kufuatilia maendeleo ya watoto wetu. Aidha, nawapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi. Napenda kuchukua fursa hii, kuwahimiza kuendelea kufanya bidii katika kujifunza ili waweze kufanikiwa kujiunga na mafunzo ya elimu ya juu baada ya kuhitimu Kidato cha Sita na Vyuo vya Elimu na ya Ufundi.

Ninawashukuru Viongozi na Watendaji wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Wananchi kwa ujumla kwa kushiriki kikamilifu kuimarisha miundombinu

ya Shule ikiwemo mabweni na majengo mengine yaliyowezesha Shule kupokea wanafunzi wote waliopangwa Kujiunga na Kidato cha Tano.

**Ndugu Wanahabari;**

Nitumie pia fursa hii kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kuwa na Shule za Sekondari za Kidato cha Tano katika kila Tarafa inatekelezwa ili kuwezesha wanafunzi wote wanaofaulu Mtihani wa Kidato cha Nne kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano na Sita. Upanuzi na ujenzi wqa Shule Mpya za Kidato cha Tano na Sita uendelee kufanyika ikiwa ni pamoja na kuongeza tahasusi za masomo ya sayansi**.** Mikoa ihakikishe inakuwa na tahasusi zote za msingi katika Shule zake ili kuwapunguzia wazazi/walezi gharama za usafiri kwenda Shule za mbali

Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi mwaka, 2023 inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ya selform.tamisemi.go.tz na Baraza la Taifa la Elimu ya Mafunzo ya Ufundi ya www.nacte.go.tz**.**

**Ndugu Wanahabari;**

Pamoja na maelekezo haya, kwa mwanafunzi, mzazi/mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelekezo au ufafanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri au apige simu kwenye namba ya Kituo cha Mawasiliano cha OR-TAMISEMI kwa **namba za simu 026 2160210 au 0735 160210.**

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Mhe. Angellah J. Kariuki, (**MB**)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS -TAMISEMI.**

**11.06.2023**